NBAA
BODI YA TAIFA YA WAHASIBU NA WAKAGUZI WA HESABU
TANZANIA

IDARA YA MITIHANI NA MAFUNZO

MASWALI YANAYOULIZWA MARA KWA MARA

1. **Nimemaliza elimu ya sekondari hivi karibuni. Je, ni kozi zipi ninazoweza kuchukua?**
   JIBU: NBAA ni taasisi ya kutahini na huwa hakiendeshi kozi zozote za uhasibu bali hushirikiana na vyuo vinavyoendesha masomo ya uhasibu ambavyo inavitambua ili viendeshe mafunzo hayo kwa wanafunzi wanaojiandaa kwa mitihani ya Bodi.

2. **Ni mitihani gani inayoendeshwa na NBAA?**
   JIBU: NBAA inaendesha mitihani katika ngazi mbili za kitaaluma; Mitihani kwa ajili ya Cheti cha Uandishi na Utunzaji Vitabu vya Hesabu Ngazi ya I & II (Accounting Technician Examinations – ATEC Level I & II) yenye masomo manne manne kila ngazi na Mitihani ya Kitaaluma ya Uhasibu – Professional Examinations ambapo mhitimu hupata shahada ya Uhasibu yaani Certified Public Accountant (CPA). Mitihani ya ATEC iko katika ngazi mbili ; ATEC 1 na ATEC II. Mitihani ya CPA iko katika hatua tatu ; Ngazi ya Msingi yenye masomo matano, Ngazi ya Kati yenye masomo sita na Ngazi ya Mwisho yenye masomo manne.

3. **Masharti ya kujiunga kufanya mitihani ya ATEC I ni yapi?**
   JIBU: Masharti ya kujiunga katika mitihani ya ATEC ni kuwa na cheti cha kumaliza elimu ya Sekondari na kufaulu vizuri (credit) masomo yasiyopungua matatu (3) na kufaulu (pass grade) masomo mawili (2) ikiwemo Kiingereza na Hisabati.

   AU cheti cha kumaliza elimu ya sekondari kidato cha sita (VI) na kufaulu masomo makuu mawili au moja na somo la ziada, alimradi uwe umefaulu Hisabati katika Elimu ya Sekondari ya Kidato cha nne (IV) angalau kwa alama ya D.

AU Cheti cha mwaka mmoja kutoka chuo kinachotambulika pamoja na ufaulu wa alama ya D au zaidi katika masomo ya Kiingereza na Hisabati katika cheti cha kidato cha nne

AU Vyeti vingine ambavyo vitakavyoendelea kutambuliwa na Bodi wakati kwa wakati.

4. Je nikiwa sina masomo matatu niliyofaulu vizuri (credit) katika elimu ya Sekondari, lakini napenda kujiunga katika fani ya uhasibu, nifanye nini?

JIBU: Kuna vyeti vingine vinavyotambuliwa na NBAA : kama cheti cha NABE hatua ya II na kufaulu masomo yasiyopungua manne uliyofaulu vizuri (passes grade) pamoja na cheti cha kidato cha nne(IV).

AU Barua ya Matokeo ya Hatua ya Msingi ikionyesha kuwa umefaulu mtihani huo ambao unaendeshwa na **Bodi ya Taifa ya Usimamizi wa Vifaa.** Zaidi ya hayo ni lazima uwe umemaliza elimu ya Sekondari ikionyesha masomo uliyofanya na kufaulu.

5. Nina Cheti cha Elimu ya Sekondari chenye masomo matano ya 'credit' lakini sina 'credit' katika Kiingereza na Hisabati. Je nifanye nini?

JIBU: Ni muhimu kwa watahiniwa wote kuwa na uwezo wa kuandika na kuongea Kiingereza na uwezo wa kushughulikia mbinu za Hisabati. Hii itakusaidia kukujengea msingi wa kutosha katika kozi uliyochagua kusoma na kufanya mitihani.

Ili uweze kukubaliwa kusajiliwa na Bodi, utahitajika au kurudia mtihani wa elimu ya Sekondari au kufanya mitihani mingine iliyotajwa hapo juu ili uweze kufikia kiwango kinachohitajika.

6. Nini masharti ya kujiunga na mitihani ya ATEC II?

JIBU: Masharti ya kujiunga ni kuwa na cheti cha kumaliza elimu ya sekondari kidato cha sita (VI) na kufaulu masomo makuu mawili na somo la ziada, alimradi uwe umefaulu Hisabati katika Elimu ya Sekondari ya Kidato chan nne (IV).

Vile vile kuna sifa nyinginezo ambazo zinatambulika na Bodi, ambazo zinakuwezesha kuanza na ATEC II nazo ni :

Barua ya matokeo ya kufaulu ATEC I

AU Cheti cha Uandishi wa Vitabu vya Hesabu : NABOCE **(mtihani hautahiniwa kwa sasa na Bodi**

AU Diploma ya Ugavi iliyokuwa inayotolewa na PSPTB

AU Cheti ya Uhasibu/Cheti cha Uhasibu Serikalini kitolewacho na Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA)

AU Certificate in Financial Administration (CFA) kitolewacho na Zanzibar Institute of Financial Administration

AU Diploma ya miaka miwili (isiyo ya Uhasibu) kutoka katika chuo kinachotambulika.

AU Cheti cha Uhasibu na Uongozi kitolewacho na SMMCo

AU Diploma/Diploma ya Juu ya Customs na Tax Management itolewayo na Chuo cha Kodi ambapo kuna msamaha wa somo kwa somo.

AU Mhitimu wa Kidato cha Sita aliyesoma mchepuo wa Biashara

AU Mhitimu wa Kidato cha Sita aliyesoma mchepuo wowote lakini alisoma na kufaulu masomo ya Biashara katika elimu ya Sekondari katika O-level.

NB : Mhitimu pamoja na sifa hizo juu anahitajika kuwa amefaulu kidato cha nne masomo ya Hesabu na Kiingereza kwa alama D au zaidi.

7. Je, naweza kujiandaa kwa mitihani kwa muda gani?

JIBU: Ili kukamilisha ipasavyo muhtasari wa masomo yanayotakiwa, mtahiniwa anatakiwa kufanya mafunzo yasiyopungua miezi tisa au kuhudhuria vipindi viwili vya mazoezi ya kurejea (review classes).

8. Je, naweza kuruhusiwa kufanya mitihani ya ya ngazi ya chini na ya juu kwa wakati mmoja?

JIBU: Hapana, unatakiwa kwanza ufaulu ATEC I kabla ya kuendelea na ATEC II. Lakini katika kipindi hiki cha mpito mtahiniwa ataruhusiwa kujisajili katika ngazi mbili tofauti endapo atakuwa amebakiza somo moja au mawili katika ngazi ya chini.

9. Je, ada za mitihani ya Bodi ni zipi?

JIBU Ada mbalimbali za mitihani ya Bodi ni kama ifuatavyo :

S/N.	Service Item	Rate/Fee	
1.	Examination Fees (single subject) • Textbook for ATEC = 30,000. • Text book for Professional = 40,000 **NB:** Repeated subject no payment for a book	ATEC I ***Repeated subject***	Shs.55,000.00 ***Shs.25,000.00***
		ATEC II ***Repeated subject***	Shs.60,000.00 ***Shs.30,000.00***
		Foundation ***Repeated subject***	Shs.100,000.00 ***Shs.60,000.00***

		Intermediate ***Repeated subject***	Shs.130,000.00 ***Shs.90,000.00***
		Final ***Repeated subject***	Shs.150,000.00 ***Shs.110,000.00***
2.	Exemption Fees (single subject)	ATEC I ATEC II Foundation	Shs.15,000.00 Shs.20,000.00 Shs.30,000.00
3.	Applicable Registration Fee at each Examination Level	ATEC I	FORM FEE - Shs. 20,000.00 REG. FEE - Shs. 25,000.00 SASF - Shs. 35,000.00 Total - **shs. 80,000.00**
		ATEC II	FORM FEE - Shs. 20,000.00 REG. FEE - Shs. 25,000.00 EXEMP. - Shs. 45,000.00 SASF - Shs. 35,000.00 Total - **shs125,000.00**

		FOUNDATION LEVEL	FORM FEE - Shs. 20,000.00 REG. FEE - Shs. 50,000.00 EXEMP. - Shs105,000.00 SASF - Shs. 70,000.00 Total - **Shs.245,000.00**
		INTERMEDIATE LEVEL	FORM FEE - Shs. 20,000.00 REG. FEE - Shs. 50,000.00 EXEMP. - Shs. 205,000.00 SASF - Shs. 70,000.00 Total - **Shs.345,000.00**
4.	Annual Subscription Fees	ATEC Professional	Shs.35,000.00 Shs.70,000.00
5.	Preparation of Transcript (per examination level)	ATEC Professional	Shs.35,000.00 Shs.40,000.00
6.	Preparation letter of Recommendation (per examination level)	ATEC Professional	Shs.10,000.00
7.	Loss/renewal of ID fee	ATEC Professional	Shs.20,000.00
8.	Certification of certificate	ATEC Professional	Shs.20,000.00

9.	Statement of result fee	ATEC Professional	Shs.15,000.00
10	Appeal fee (per subject)	ATEC Professional	Shs.160,000.00
11	Search fee	ATEC Professional	Shs.25,000.00
12	Convocation Fee	All Graduates (Examination certificate cover)	Shs.20,000.00
13	Late collection of certificates	All levels	Shs.20,000.00@ exceeding six months after graduation
14	Mid examinations	A5 Business Law B4 Public Finance & Taxation I C4 Public Finance & Taxation II	Shs.450,000.00 Shs.500,000.00 Shs.550,000.00
15.	Non Citizens		To be charged twice [the rate pegged in US $]

10. Je, naweza kulipa ada zilizotajwa hapo juu kwa awamu?

JIBU: Ndiyo, unaweza kulipa ada hizi kwa awamu kwa mpangilio ufuatao: ada ya usajili, ada ya msamaha wa masomo (exemptions) na ada ya mwaka yalipwe kwanza halafu ada za mitihani baadaye. Hata hivyo, malipo haya ni lazima yafanywe kabla ya tarehe za mwisho za kulipia ambazo ni 31 Januari na 31 Julai kwa wale wanaofanya usajili kwa mara ya kwanza, malipo ya mtihani yafanyike kabla ya tarehe 15 Machi na 15 Septemba kwa mitihani ya Mei na Novemba.

11. Je, nitalipaje ada?

JIBU: Malipo yafanywe kwa kupitia tawi lolote la CRDB kwenye Account No. 01J 100 555 3500 – ya NBAA iliyopo Tawi la CRDB Vijana, Barabara ya Lumumba, DSM. Huna budi kuzingatia kuwa fomu ya kuwekea (Pay-in-slip) lazima iwasilishwe Bodi pamoja na fomu za maombi ya usajili au ya mtihani. Risiti halisi ya malipo kupitia benki ndiyo inayotakiwa.

12. Je, mtihani wa kitaaluma (Professional Examinations) una hatua ngapi?

JIBU: Mtihani wa kitaaluma umegawanyika katika hatua tatu: Hatua ya Msingi (Foundation Stage). Hatua ya Kati (Intermeiate Level) na Hatua ya Mwisho (Final Level). Kwa jumla kuna masomo 15 ya kutahiniwa.

13. Iwapo mimi ni mwanafunzi wa mwaka wa kwanza au wa pili au wa tatu katika chuo cha elimu ya juu au nimeachishwa masomo kabla ya kumaliza programu yangu, je nitaweza kuanzia katika ngazi gani katika mitihani ya kitaaluma (professional examinations?) Na je, nitapata misamaha gani katika masomo ya ngazi hizo?

JIBU: Bodi haitoi misamaha kwa programu ambazo mwanafunzi hakuweza au hajamaliza. Unatakiwa kukamilisha kabisa programu unayochukua ili sifa uliyoipata iweze kufanyiwa tathmini. Lakini iwapo umekatishwa masomo kabla ya kukamilisha programu yako, sifa uliyopata kabla ya kujiunga na chuo cha elimu ya juu itatuongoza kutathmini ni katika ngazi gani ya mitihani ya NBAA utakayoweza kuanzia.

14. Ni sifa zipi ambazo zinahitajika ili kuweza kufanya mitihani ya kitaaluma?

JIBU: Mtahiniwa anastahiki kufanya mitihani ya kitaaluma iwapo ana sifa zifuatazo, zinazolinganishwa na ngazi mbali mbali za mitihani itolewayo na NBAA.

14.1 Hatua ya Msingi (Foundation Level):

Cheti cha Uandishi na Utunzaji wa Vitabu vya Hesabu Ngazi ya pili (ATEC II).

Taasisi inayotoa: NBAA

AU Diploma ya Uhasibu/uhasibu na fedha kutoka katika chuo kinachotambulika

AU Stashahada ya Juu ya miaka mitatu/Shahada kutoka katika chuo kinachotambulika, isiyokuwa ya uhasibu itolewayo na vyuo vya elimu ya juu: kwa mfano: Bsc.Eng. Bsc. Mathematics, B. Com. Finance, B. Com. Marketing, Stashahada ya Juu ya Usimamizi wa Usafirishaji n.k.

Msamaha wa somo kwa somo utatolewa kwa kuangalia ni masomo gani mwanafunzi atakuwa amekazia maarifa (specialization).

14.2 Hatua ya Kati (Intermediate Level)

Barua ya Matokeo ya Kufaulu hatua ya msingi (Foundation Level)

Taasisi inayotoa: NBAA

AU Stashahada ya Juu ya miaka mitatu/Shahada ya uhasibu /uhasibu na fedha kutoka katika chuo kinachotambulika, itolewayo na vyuo vya elimu ya juu

14.3 Hatua ya mwisho (Final Level)

Cheti cha hatua ya kati (Intermediate Stage certificate)
Taasisi inayotoa: NBAA

14.5 Programmu zinazotambuliwa na Bodi ambazo wahitimu wake wana sifa za kuanza mitihani ya Bodi katika ngazi ya kati:

Shahada ya Biashara - (Uhasibu).
Taasisi inayotoa: UDSM
Stashahada ya Juu katika Uhasibu (ADCA), Shahada ya Uhasibu na Fedha; Bechelor of Public Sector Accounting and Investigations (B. PSAI).
Taasisi Inayotoa: MU
Stashahada ya Juu katika Uhasibu (ADA).
Shahada ya Uhasibu
Taasisi inayotoa: IFM
Stashahada ya Juu katika Uhasibu (ADA).**Utambuzi ni kuanzia 1993**
Shahada ya Uendeshaji wa Biashara (Uhasibu) (BBA – Accounting)
Taasisi Inayotoa: SAUT,
Shahada ya Juu katika Uhasibu wa Ushirika (ADCA). **Utambuzi ni kuanzia 1993**
Shahada ya Sanaa (Uhasibu na Fedha)
Shahada ya Sanaa katika uendeshaji wa ushirika na uhasibu
Taasisi inayotoa: MUCCoBS
Stashahada ya Juu katika Uhasibu (ADA).
Shahada ya Uhasibu
Taasisi Inayotoa: IAA.
Stashahada ya Juu katika Uhasibu (ADA)
Shahada ya Juu katika Uhasibu wa Serikali (ADGA). ***utambuzi ni kuanzia 1999***
Shahada ya Uhasibu
Taasisi Inayotoa: TIA
Stashahada ya Juu katika Uhasibu ***utambuzi ni kuanzia 2000***
Shahada ya Uhasibu
Taasisi Inayotoa: CBE
Stashahada ya Juu katika Uendeshaji wa Fedha (ADFA).
Taasisi Inayotoa: ZIFA.

Stashahada ya Biashara (Uhasibu)
Shahada ya Uendeshaji wa Biashara (Uhasibu)
Taasisi Inayotoa: OUT.
Shahada ya Uendeshaji wa Biashara (Uhasibu
Taasisi* Inayotoa*: ZU.
Shahada ya Uendeshaji wa Biashara (Uhasibu).
Taasisi Inayotoa: TU-DSM College – Utambuzi kuanzia mwaka wa masomo 2007/08
*Shahada ya Uendeshaji wa Biashara (Uhasibu)****Utambuzi ni kuanzia mwaka wa masomo 2004/05.***
Shahada ya Sayansi ya Uhasibu
Taasisi Inayotoa: TU – Iringa College
Shahada ya Uhasibu
Stashahada ya Uhasibu, ***Utambuzi kuanzia 2007/8***
Taasisi inayotoa: (SMMUCO).
Shahada ya Uendeshaji wa Biashara
Shahada ya Uhasibu na Fedha
Taasisi inayotoa: St. John's University of Tanzania
Shahada ya Uendeshaji wa Biashara
Taasisi inayotoa:UoA
Shahada ya Uendeshaji wa Biashara
Taasisi inayotoa:MT. Meru university.
Shahada ya Sayansi ya Uhasibu na Fedha
Taasisi inayotoa: ARU
Shahada ya uendeshaji wa Biashara (Uhasibu)
Taasisi inayotoa: UDOM
Shahada ya Uhasibu
Taasisi inayotoa: TEKU
Shahada ya Uendeshaji wa Biashara
Taasisi inayotoa:Ruaha university

15. Je, inachukua muda gani kwa mtahiniwa kumaliza CPA (T)?

JIBU: Inategemea uwezo wa mtu na ngazi mtahiniwa aliyoanzia. Kwa mfano, mhitimu wa Shahada ya Juu ya Uhasibu anaweza kuchukua muda mfupi kumaliza kuliko yule aliyeanzia katika hatua ya kwanza yaani foundation stage. Vile vile kumaliza mitihani ya CPA kunategemea juhudi na bidii ya mtahiniwa mwenyewe. Mtahiniwa mwenye bidii na matayarisho mazuri katika masomo yake ana nafasi kubwa ya kufaulu na kuendelea na mitihani mingine kuliko yule ambaye inabidi arudie-rudie mitihani baada ya kushindwa kufaulu.

16. Tuchukulie kwamba nimejiandikisha kwa mitihani lakini kutokana na sababu zisizozuilika nimeshindwa kufanya mtihani, je naweza kurudishiwa fedha?

JIBU: Hapana. Mara ada ikilipwa hairudishwi ingawa inaweza kutumika kwa mitihani ijayo iwapo kuahirishwa/kujitoa huko kulifanywa kabla ya tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya kufanya mtihani.

17. Ni kina nani wanaoendesha mafunzo na ni wapi naweza kuchukua mafunzo hayo?:

JIBU: Vituo vya kuendesha mafunzo ni vingi hasa katika mji wa Dar es Salaam. Vituo hivi vya mafunzo vinavyotambuliwa na Bodi hutoa masomo ya marudio au mazoezi katika kuwaandaa watahiniwa kwa mitihani ya Bodi. Iwapo unataka kujisajili katika vituo hivyo tafadhali soma kipeperushi "Tuition Providers' Directory au soma kwenye tovuti ya Bodi. Kipeperushi hiki kitakupatia taarifa ni wapi vituo hivi vinapatikana na ni katika ngazi gani hutoa mafunzo hayo.

18. Tumeelezwa kwamba Bodi inarekebisha mfumo na mitaala ya masomo ya mitihani yake je, ni lini mitaala mipya wa masomo itaanza kutumika?

JIBU: Mitaala ya Bodi hubadilika kila baada ya miaka mitano. Mitaala inayotumika hivi sasa ilianza kutumika kuanzia Novemba 2014.

19. Je, kuna upendeleo maalumu kwa waombaji walemavu au wenye mahitaji maalumu?

JIBU: Wakati Bodi inatambua mahitaji ya walemavu na kudhamiria kuwasaidia kufanya na kumaliza mitihani yao kadri iwezekanavyo, Bodi itaendelea kufuata maagizo ya Serikali kama yanavyotolewa mara kwa mara kwa ajili ya kwasaidia walemavu.

20. Je, naweza kuwasilisha fomu yangu ya usajili au fomu ya kuomba kufanya mtihani kwa waendeshaji masomo ya kujiandaa kwa mitihani (Tuition Providers) wanaotambuliwa na NBAA?

JIBU: Watahiniwa wanashauriwa kuwasilisha fomu zao za usajili wa mitihani katika Ofisi za Bodi zilizopo katika Jengo Mhasibu chumba Na. S03. Hii itakupa uhakika kuwa fomu zako zimefika. Hata hivyo hukatazwi kutumia njia nyingine ili mradi uhakikishe kuwa maombi yako yamewasilishwa.

Vile vile fomu hizo zinaweza kutumwa kwa njia ya posta.

21. Je, machapisho ya NBAA na nyenzo za kujifunzia zinapatikana katika mahali gani?

JIBU: Machapisho yanapatikana katika Duka la Vitabu la NBAA na katika maktaba yake ya marejeo yenye vitabu vilivyoorodheshwa katika Muhtasari wa Mafunzo. Duka la Vitabu na Maktaba vyote vipo katika Jengo la Mhasibu.

22. Nataka kujisajili na Bodi na baadaye kufanya mitihani. Je nitapata wapi fomu?

JIBU: Fomu za Usajili wa Mtahiniwa (Candidacy Registration Fomu na Fomu za Kujiunga na Mitihani zinaweza kunakiliwa kutoka Tovuti ya NBAA, kwa kutumia: www.nbaa.go.tz/examinations/forms

23. Je kama mimi nimesoma nje ya nchi na nina Cheti/Diploma ya Uhasibu/Stashahada ya juu katika Uhasibu/Shahada ya Uhasibu, naruhusiwa kujisajili kufanya mitihani ya NBAA?

JIBU: Ndiyo. Unachohitajika kufanya ni Kujaza fomu ya Usajili (Candidacy Registration and Exemption form) kutoka katika tovuti ya NBAA. Wasilisha fomu yako kwenye ofisi ya Usajili NBAA au tuma kwa njia ya Posta. Fomu hiyo iambatanishwe na:

(i) Barua kutoka Tanzania Commission for Universities (TCU) kwa ajili ya kupata utambulisho rasmi wa chuo ulichosoma na cheti ulichopata,

(ii) Vivuli vya vyeti vyako vyote toka elimu ya sekondari mpaka elimu ya juu. Vyeti hivyo viwe vimethibitishwa na hakimu au wakili wa kujitegemea kuwa ni nakala halisi.

Au uthibitisho huu unaweza kufanyika hapa hapa NBAA wakati wa kujisali ikiwa utaamua kuja mwenyewe.

(iii) Picha zako tatu passport size ambazo zimepigwa hivi karibuni.

(iv) Mtaala wa mafunzo uliyochukua (syllabus)

Fomu za usajili pamoja na viambatisho vyote viwasilishe NBAA kwa pamoja – aidha kwa njia ya posta au kwa kuja wewe binafsi.

24. Mimi nimemaliza mafunzo yangu ya taaluma ya uhasibu nje ya nchi au nimesoma taaluma kama hiyo nikiwa hapa nchini lakini inatolewa na nchi nyingine. Je nitakuwa sawa na mhasibu aliyemaliza CPA ya Tanzania?

JIBU: Ili uweze kuwa sawa na mhasibu aliyefuzu taaluma ya uhasibu ya Tanzania ni lazima ufanye masomo mawili ya kodi (Public Finance and Taxation I & II) na lile la sheria ya biashara (Business Law) yaliyoko katika mtaala wa Bodi.

25. Je ninawezaje kujisajili na kufanya mitihani ya masomo hayo yaliyotajwa hapo juu?

JIBU: Ili kuleta ufanisi na kuruhusu mhusika afanye mitihani hiyo kwa wakati unaomfaa Bodi imeanzisha mitihani ya katikati itakayofanyika katika miezi ya Februari na Augusti. Mitihani hii itawahusu wale wote wenye Shahada ya Juu ya Uhasibu ya nje pamoja na wale watahiniwa

wa Bodi ambao watakuwa wamebakiza somo moja kati ya hayo kwenye ngazi husika.

26. Kuna faida gani kwa mwanafunzi kuamua kujiunga na masomo ya CPA ya Tanzania ukilinganisha na yule aliyeamua kujiunga na masomo ya CPA ya nje?

JIBU: Kuna faida nyingi sana za kufanya CPA ya Tanzania na hatimaye kuwa Mhasibu au Mkaguzi wa hesabu au mtaalamu wa mambo ya fedha na kodi kwa kusomea CPA ya Tanzania.

No.	CPA ya Tanzania	Maelezo
1.	Utapata usajili wa moja kwa moja kuwa mwanachama wa Bodi	Ili kupata usajili kwenye Bodi ni lazima mhitimu wa fani ya nje afanye masomo matatu yaliyoko kwenye mtaaala wa Bodi kama yalivyotajwa hapo juu
2.	Kutambulika na waajiri baada ya kumaliza mitihani yako	Ni rahisi kwa mhitimu aliyemaliza CPA ya Tanzania kupenya katika soko la ajira kuliko aliyehitimu CPA nyinginezo kwa vile mwajiri anahitaji kumwajiri mtumishi anayejua sheria za kodi za Tanzania pamoja na sheria za biashara za Tanzania
3.	Utapata uhakika wa moja kwa moja wa kupata ajira nchini na katika soko la Afrika Mashariki kwa urahisi	Kutokana na maelewano yaliyopo (memorandum of understanding) kati ya nchi za Afrika ya Mashariki ni rahisi kwa mhitimu wa CPA ya Tanzania kupata ajira kwa urahisi katika nchi hizo.
4.	Utakuwa umedumisha uzalendo kwa kusoma taaluma inayotolewa nchini mwako	Unaposoma taaluma za nchi nyingine wakati taaluma hiyo hiyo inapatikana katika nchi yako inarudisha nyuma moyo wa uzalendo.
5.	Utakuwa umechangia pato la Taifa kwa ulipaji wako wa ada za mitihani katika chombo cha Taifa lako	Unapolipa ada za mitihani kwa taasisi nyingine ina maana kwamba unachangia maendeleo ya ukuaji wa uchumi wan chi nyingine badala ya kuchangia uchumi wa nchi yako
6.	Ada kwa ajili ya usajili pamoja na mitihani ya Bodi	Kwa kawaida ada za mitihani za taasisi nyingine hasa za nje ni

	ni rahisi ukilinganisha na ada za taasisi nyingine	kubwa ukilinganisha na ada za mitihani ya CPA ya Tanzania. Hii inatokana na kwamba serikali nayo inachangia kwa kiasi fulani gharama hizo.
7.	NBAA ni chombo chenye hadhi ya kisheria (Legal backing) kwani kimeundwa na sharia ya Bunge.	Taasisi nyingi za nje zinazoendesha mitihani yake kimataifa ni taasisi zilizoundwa na wanachama (associations). Hii ni tofauti na NBAA ambayo imeundwa kwa sheria ya Bunge.
8	Ukimaliza CPA utasajiliwa na NBAA kama Mhasibu au Mkaguzi wa hesabu baada ya kupata uzoefu	Ukiwa na sifa za nje, kabla hujasajiliwa na NBAA kuwa mhasibu au mkaguzi hesabu, itabidi ufanya mitihani isiopungua mitatu ya NBAA, ukifaulu ndio usajiliwe na kuruhusiwa kufanyakazi Tanzania kwa mujibu wa sheria.

27. Je ili cheti cha kumaliza chuo kiendelee kutambuliwa na Bodi ninatakiwa nifanye nini?

JIBU: Ili cheti chako kiendelee kutambuliwa na Bodi ni lazima ujisajili kwa mitihani ndani ya miaka miatno tangu ulipohitimu mafunzo husika. Endapo hutafanya hivyo basi itabidi uanzie ngazi ya chini. Mfano badala ya kuanza na ngazi ya kati (Intermediate) utalazimika kuanza na ngazi ya awali (Foundation). Bodi inaweza kukufikiria kukupa msamaha endapo baada ya kuhitimu masomo yako ulienda kusoma kozi ingine ya masomo.

28. Nawezaje kufahamu tarehe za usajili kwenye mitihani ya Bodi?

JIBU: Kuna tarehe za aina tatu. Aina ya kwanza mwanafunzi analipa ada ya mitihani pamoja na usajili bila faini. Aina ya pili mwanafunzi analipia na faini ya asilimia hamsini na aina ya tatu mwanafunzi/mtahiniwa analipia na faini ya asilimia mia moja. Tazama jedwali hapa chini kwa ufafanuzi.

Muundo wa malipo	**Mitihani ya Mei**	**Mitihani ya Novemba**
Malipo ya ada bila faini	02 – 31 Januari	01 – 31 Julai
Kwa malipo ya faini asilimia 50	01 – 28 Februari	01 – 30 Augusti
Kwa malipo ya faini asilimia 100	01 – 31 Machi	01 – 30 Septemba

29. Je naweza kulipa ada ya usajili pamoja na ada ya mitihani kwa wakati mmoja?

JIBU: Wanafunzi/watahiniwa wanashauriwa kujaza fomu na kulipia usajili pamoja na mitihani kwa wakati mmoja ili kuweza kupata vitabu

mapema kwa ajili ya kujiandaa kwa mitihani. Mtahiniwa ili aweze kupatiwa vitabu ni lazima ajaze fomu ya mitihani pamoja na kulipia mitihani husika.

30. Ni kwa namna gani ninaweza kupata vitabu vya kusoma baada ya kulipia masomo kwa ajili ya mitihani?

JIBU: Baada ya fomu ya mwanafunzi/mtahiniwa kufika Bodi ikiwa imeambatanishwa na risisti ya malipo ya benki; Bodi itatuma vitabu vya mhusika moja kwa moja kwenye sanduku lake la posta. Hivyo wanafunzi/watahiniwa wanshauriwa kuandika anwani sahihi wanapojaza fomu za mitihani. Wanafunzi/watahiniwa wa mitihani walioko Dar es Salaam wao vitabu vyao havitatumwa kwao bali watatatikiwa kuja wenyewe kuvichukua katika dula la vitabu lililopo Mhasibu House.

31. Je ninaweza kujisajili kufanya masomo katika ngazi mbili tofauti?

JIBU: Mwanafunzi/mtahiniwa aliyebakiza masomo kadhaa katika ngazi ya chini anaruhusiwa kujisajili kwa ajili ya masomo hayo pamoja na masomo yaliyopo ngazi ya juu yake hali mradi jumla ya masomo atakayojisajili kwa ajili ya mtihani huo yasizidi matano. Mfano unaweza ukajisajili masomo matatu ngazi ya awali na masomo mawili ngazi ya kati nakadhalika.

32. Je ni wapi ninaweza kusoma au kupata vitabu vya rejea kwa ajili ya kujiandaa kwa mitihani:

JIBU: Bodi ina maktaba yenye vitabu mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi/watahini kwa ajili ya mitihani. Maktaba hiyo iko katika jingo la Mhasibu House. Ukshajiandikisha kama mtahiniwa unaruhusiwa kutumia maktaba hii. Pia lipo duka la vitabu ambalo huuza vitabu kwa bei nafuu kwa ajili ya wadau mbalimbali wakiwepo watahiniwa wa mitihani. Duka hili pia lina vijarida vya maswali na majibu ya mitihani iliyopita.

33. Mimi nimemaliza mafunzo yangu ya taaluma ya uhasibu nje ya nchi kama ACCA, CIMA, SAICA, ICAEW nk. na shahada yangu ya kwanza ya uhasibu nilisoma hapa nchini. Je nitakuwa sawa na mhasibu aliyemaliza CPA (T)?

JIBU: Ili uweze kuwa sawa na mhasibu aliyefuzu taaluma ya uhasibu ya Tanzania ni lazima ujisajili na kufanya masomo mawili ambayo ni Public Finance and Taxation I & II.

34. Mimi nimemaliza mafunzo yangu ya taaluma ya uhasibu nje ya nchi kama ACCA, CIMA, SAICA, ICAEW nk. na shahada yangu ya kwanza ya uhasibu nilisoma nje ya nchi. Je nitakuwa sawa na mhasibu aliyemaliza CPA (T)?

JIBU: Ili uweze kuwa sawa na mhasibu aliyefuzu taaluma ya uhasibu ya Tanzania ni lazima ujisajili na kufanya masomo matatu ambayo ni Business Law na Public Finance and Taxation I & II.

35. Mimi nimelipia mitihani ya Bodi kabla ya tarehe ya kufunga usajili lakini nikatuma fomu yangu na risiti ya benki baada ya siku ya usajili. Je nitatakiwa kulipia faini/penalty?
    JIBU: Hapo ni lazima utalipishwa faini kwa vile kinachozingatiwa zaidi ni fomu ya usajili ifike Bodi kabla ya tarehe ya mwisho ya usajili.

36. Je nikishasajiliwa kama mtahiniwa wa mitihani ya Bodi nitatakiwa kufanya nini cha zaidi mbali na kujisajili kufanya mitihani?
    JIBU: Utatakiwa kulipa ada za kila mwaka (subscription fee) ambayo hulipwa kuendana na kalenda ya mwaka (Janauri-Disemba). Wale wa ngazi ya Cheti Accounting Technician hutakiwa kulipa shs.25,000 kila mwaka na wale wa ngazi ya Taaluma ya Juu ya uhasibu (professional level) hutakiwa kulipa shs.50,000 kila mwaka.
37. Je nimepoteza kitambulisho nitafanyeje?
    JIBU: Utatakiwa kupakua fomu iliyoko kwenye tovuti ya Bodi na kuijaza na kuambatanisha na picha tatu (passport photo) ulizopiga hivi karibuni pamoja na risiti ya benki ya malipo ya shs.20,000.
38. Je nikitaka kuomba transcript taratibu zikoje?
    JIBU: Utatakiwa kupakua fomu iliyoko kwenye tovuti ya Bodi imeandikwa 'Request for Transcript' na kuambatanisha na picha mbili (passport photo) ulizopiga hivi karibuni pamoja na risiti ya benki ya malipo ya shs.30,000 kwa kila hatua/level ya 'professional examinations' au shs.25,000 kwa kila hatua/level ya mitihani ya cheti/accounting technician.
39. Je ninaruhusiwa kufanya kujisajili na kufanya mitihani ya Bodi kama mtahiniwa binafsi?
    JIBU: Bodi hairuhusu mtu yeyote kujisajili na kufanya mitihani bila kusoma katika vituo vya kufundishia (review classes) vilivyosajiliwa na Bodi. Bodi huwaruhusu tu wale wanafunzi/watahiniwa ambao wako katika mikoa ambayo hakuna vituo vya kufundishia.
40. Je nikishasajiliwa nitapata namba ya usajili baada ya muda gani?
    JIBU: Bodi huanza kushughulikia fomu za usajili baada ya kufunga zoezi la usajili. Baada ya hapo barua za usajili huanza kutumwa kwa watahiniwa kupitia kwenye anwani zao.
41. Je nikishasajiliwa kufanya mitihani ya Bodi nitapata kitambulisho baada ya muda gani?
    JIBU: Vitambulisho hutolewa siku moja kabla ya mitihani husika kuanza kwa watahiniwa wa mkoa wa Dar es Salaam. Wale watahiniwa wa mikoani hupatiwa vitambulisho vyao siku moja kabla ya mitihani kwenye vituo walivyopangiwa kufanyia mitihani.
42. **Naweza kupata wapi habari zaidi kuhusu NBAA**
    JIBU: Unaweza kupata taarifa/habari zaidi kuhusu NBAA kwa kupitia njia zifuatazo:-

Mkurugenzi Mtendaji,

Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu,
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed,
S. L. B. 5128,
Dar es Salaam,
Tanzania.
Barua pepe: info@nbaa.go.tz
Wavuti: www.nbaa.go.tz
Simu ya mezani: +255 (22) 2211890/9
Simu ya kiganjani: 0736-218031
Nukushi: +255 (22) 2151746